# OFISI YA RAIS -TAMISEMI
# HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

**SHULE YA SEKONDARI LUPEMBE**
**S.L.P 114,**
**NJOMBE**
**27/11/2020**

**SIMU: 0758216754 -MKUU WA SHULE**
**0745298729 -M/MKUU WA SHULE**

**Kumb JNG/LSS/OL/2021/............**

**MZAZI/MLEZI WA.............................................................**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUPEMBE KIDATO CHA KWANZA 2021.**

Tunayo furaha kukuarifu kuwa mtoto wako ................................................... mwenye namba ya mtihani ..........................................Amechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika Shule hii Januari 2021. Mtoto wako anatakiwa kufika siku ya Jumatatu **tarehe 11/01/2021** kwa ajili ya kuanza masomo. Muhula wa kwanza wa Masomo utaanza tarehe **11/01/2021**. Hivyo utapaswa kufika kwa wakati. Shule ya Sekondari Lupembe ipo umbali wa kilometa sabini 70 mashariki mwa Mji wa Njombe, usafiri wa basi Tsh 5000/= kutoka kituo cha mabasi Njombe Mjini hadi mahali Shule ilipo.

***KAULI MBIU YA SHULE (SCHOOL MOTTO) "ONE STEP DOES NOT MAKE A PATH".*** Kauli mbiu hii ni dira ya mwanao kwa muda wa kipindi chote cha miaka mnne atakapokuwa hapa shuleni hivyo atatakiwa kuitafakari kauli hiyo kwa vitendo. Nimatumaini yetu kuwa mwanao atatumia nafasi hii adimu kwa manufaa yake, wazazi, umma na Taifa kwa ujumla. Hivyo mwanao atakiwa kuwa na tabia njema kuhudhuria masomo na kujifunza kwa bidiii.

Tafadhali ieleweke kwamba mtoto wako atapokelewa kwa matumaini kuwa ateendelea na masomo yake kuanzia kidato cha **kwanza** hadi kidato cha Nne. Hatutapenda kuona mtoto anakatishwa masomo kwa sababu zisizo na msingi.

- **SARE YA SHULE: WASICHANA (HATUTAKI NGUO ZA MITUMBA)**

1. Mashati mawili meupe mikono mirefu (Tetroni)
2. Vigauni daki bluu (Dark blue) viwili urefu vivuke magoti na suruali mbili rangi inayofana na vigauni.
3. Sketi rangi ya Kijani mgomba mbili kwa ajili ya kazi.
4. Tshirt na bukta za rangi ya bluu jozi mbili kwa ajili ya michezo
5. Traksuti daki bluu jozi moja (01)
6. Viatu vya ngozi nyeusi tupu (bila mabaka) vya kufunga na kamba visivyo na kisigino kirefu jozi mbili (02).
7. Raba nyeupe za michezo jozi moja.
8. Soksi nyeupe jozi nne.
9. Masweta mawilirangi ya bluu zinapatikana madukani.
10. Kofia (mzula) rangi ya bluu itavaliwa nyakati za usiku kutokana na hali ya hewa kuwa ni baridi
11. Hijabu kwa Wanafunzi wa Kike wa Kiislam ifanane na sare ya Shule.

- **SARE YA SHULE WAVULANA (HATUTAKI NGUO ZA MITUMBA)**

1. Mashati mawili meupe mikono mifupi (Tetroni)



ONE STEP DOES NOT MAKE A PATH

2. Suruali daki bluu (Dark blue) mbilizenye turnup (hatuitaji suruali za kubana)/ modo
3. Suruali nyeusi (black) mbilizenye turnup (hatuitaji suruali za kubana)/ modo zitavaliwa wakati wa kazi tu na siyo darasani.
4. Tshirt na bukta za rangi ya njano jozi mbili kwa ajili ya michezo
5. Traksuti daki bluu jozi moja (01)
6. Viatu vya ngozi nyeusi tupu (bila mabaka) vya kufunga na kamba visivyo na kisigino kirefu jozi mbili (02).
7. Raba nyeusi za michezo jozi moja.
8. Soksi nyeusi jozi nne.
9. Masweta mawili rangi ya bluu zinapatikana madukani.
10. Kofia (mzula) rangi ya bluu itavaliwa nyakati za usiku kutokana na hali ya hewa kuwa ni baridi

**NB**

- **HATUTARUHUSU SARE NYINGINE KUVALIWA NA MWANAFUNZI AWAPO SHULENI ZAIDI YA HIZO ZILIZOAINISHWA.**

❖ **MAHITAJI TAALUMA , USAFI NA AFYA.**

1. Picha za passport nakala 3 .
2. Daftari zisizopungua 10 Counter Book na kalamu zisipungue kumi.
3. Lazima aje na mkebe wa vifaa vya hesabu (Mathematical set) na rula.
4. Dictionary ya English to English.
5. Begi jeusi la kubebea daftari la kubeba mgongoni.(school bag)
6. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

**NB :**

- Vifaa vyote vitakaguliwa.
- Elimu ni urithi pekee mzazi unaoweza ukampa mtoto wako, mtimizie mahitaji yake kwa faida ya baadaye.

❖ **FOMU ZA KURUDISHA SHULENI.**

Fomu zote ziwasilishwe shuleni mara afikapo pamojaa na vifaa vyote.

(i) **Fomu A** Taarifa binafsi za Mwanafunzi.
(ii) **Fomu B** kukubali kufuata sheria za Shule na kuthibitishwa na mzazi.
(iii) **Fomu C** hati ya Daktari kuthibitisha afya yake.

Tunamtakia Mtoto wako afya njema na kazi nzuri yenye maendeleo na mafanikio wakati wowote wa kuwepo hapa Shuleni.

**Ndimi**

……………………………

**ISDORY MAHOLO**

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
LUPEMBE SEKONDARI
S. L. P. 114
NJOMBE

ONE STEP DOES NOT MAKE A PATH

***FOMU A***

# SHULE YA SEKONDARI YA LUPEMBE

## TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI-HAKIKISHA MZAZI/MLEZI TAARIFA YA MWANAFUNZI NI SAHIHI KWA MATUMIZI YA OFISI

1. Jina aliloandikishwa……………………………………………………………………………
2. Majina mengine ya nyumbani…………………………………………………………………
3. Dini……………………………………………..
4. Tarehe ya kuzaliwa……………………………………………………
5. Mahalia alipozaliwa. Kijiji……………………………………… Kata …………………………..
   Tarafa…………………….. Wilaya……………………
6. Jina la Baba…………………………………………………………………………
7. Jina la Mama…………………………………………………………………………
8. Baba yuko Hai?.................... Mama yuko Hai? ……………………………
9. Mama ana watoto wangapi? ……………………………………….
10. Wewe ni mtoto wa ngapi kwa mama?.................................................
11. Nyumbani unapoishi Kijiji……………………Kata ……………………..Wilaya……………………..
    Anuani……………..
12. Kidato ulichopokelewa………………………………………………………………
13. Shule uliyotoka………………………………………………………………………………
14. Shughuli mbali na Masomo……………………………………………………………
15. Kukiwa na Tatizo Taarifa ipelekwe kwa
    Jina ………………………………………
    Anwani …………………………………
    Uhusiano wenu …………………………
    Sahihi ya Mwanafunzi …………………….. Tarehe …………………………..

## KWA MATUMIZI YA OFISI

Namba ya kuandikishwa Shuleni…………………………………………………………………
Namba ya Mtihani……………………………………………………………………………
Mkuu waShule…………………………………………………………………………………

Bandika picha yake hapo

| PICHA |
|---|

**Ndimi**

**…………………**

**ISDORY MAHOLO**

**Mkuu wa Shule**

MKUU WA SHULE
LUPEMBE SEKONDARI
S. L. P. 114
NJOMBE

***FOMU B***

**SHULE YA SEKONDARI YA LUPEMBE**

**S.L.P 114, NJOMBE**

**YAH: KUKUBALI MASHARTI YA SHULE.**

Mimi ………………………………………………………………… Niliyechaguliwa kuendelea na Masomo Kidato cha ………………… katika Shule ya Sekondari Lupembe ninaikubali nafasi hiyo. Ninaahidi kuwa nitafuata Sheria zote za Shule zilizopo na zitakazokuja baadaye. Nitajiepusha na vitendo vyote ambavyo ni kinyume cha Sheria na taratibu za Shule. Nitakuwa mtiifu kwa Walezi wote Shuleni ambao ni Walimu na Wafanyakazi wasio Walimu.

Nitafuata maelezo nitakayopewa na Walimu na Wafanyakazi wengine wa Shule na Viongozi wote watakaokuwepo kwa mujibu wa Sheria.

Nitahudhuria vipindi vya masomo darasani na nitafanya mazoezi na mitihani yote nitakayopewa.

Ninafahamu kwamba kukiuka kwangu ahadi hii kutanipotezea nafasi yangu ya masomo.

**Sahihi ya Mwanafunzi……………………**

**Tarehe………………………………**

# AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi……………………………… Mzazi/Mlezi ……………………………………………… ninaahidi nitatoa ushirikiano mkubwa kwa Walimu na Uongozi wa Shule kuhakikisha mwanafunzi mtajwa anasoma. Na nitakuwa na Desturi ya kuja mara kwa mara shuleni kujua maendeleo ya Mtoto na kuhudhuria vikao vya Wazazi (PTA) nitakapohitajika

**Sahihi ya Mzazi/Mlezi……………………………………..Tarehe………………………**

**Namba ya Simu ……………………………………**

**Ndimi,**

………………………………………………………………………………

**ISDORY MAHOLO**

**Mkuu wa Shule.**

MKUU WA SHULE
LUPEMBE SEKONDARI
S. L. P. 114
NJOMBE

ONE STEP DOES NOT MAKE A PATH

## *FOMU C*

# FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

# LUPEMBE SECONDARY SCHOOL

# P.O. BOX 114 NJOMBE

To be completed by medical officer.

Full name ...........................................................................................................

Age ........................ Years ............................ Sex...............................................

Blood count ( Red and White)..........................................................................

Stool examination.............................................................................................

Urine analysis...................................................................................................

Syphilis test.......................................................................................................

Eye test..............................................................................................................

T.B test ..............................................................................................................

Ears ...................................................................................................................

Chest .................................................................................................................

Spleen ...............................................................................................................

Abdomen ...........................................................................................................

ADDITIONAL INFORMATION eg physical or chronical family disease,

Etc ......................................................................................................................

I certify that the above named student is fit/not fit to pursue studies

Signature

..................

Designation

.......................

Section

.........................................................................................................................

Date ................................

PUPILS: You must bring this complete form when you come to school, no pupil may enroll without certificate of physical fitness.

..........................................................................

**ISDORY MAHOLO**

**HEADMASTER**

MKUU WA SHULE
LUPEMBE SEKONDARI
S.L.P. 114
NJOMBE

**LUPEMBE SECONDARY SCHOOL**



ONE STEP DOES NOT MAKE A PATH

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na 25 ya Mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na 10 ya Mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti Shuleni.

(i) Heshima kwa viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(ii) Mahudhurio mazuri katika kila Shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima.
(iii) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni ( Night Preparation)
(iv) Kuwahi katika kila Shughuli za Shule na nyingine utakazopewa
(v) Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika Shule hii.
(vi) Kutunza usafi wa Mwili mavazi na mazingira ya Shule.
(vii) Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapotakiwa.
(viii) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote na kutunza mali ya Umma.

## MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

(i) Wizi
(ii) Uasherati na Ushoga
(iii) Ubakaji
(iv) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, Cocaine, Mirungi, kubeli na kadhalika
(v) Kupigana au kupiga
(vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(vii) Kudharau Bendera ya Taifa
(viii) Kuwa Mjamzito / kupata mimba
(ix) Kuoa au kuolewa
(x) Kutoa mimba
(xi) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani usalam wa Shule au watu
(xii) Kuwa na simu ya mkononi au viambata vyake kama betri, n.k.

……………………
Isdory Maholo
Mkuu wa Shule.

MKUU WA SHULE
LUPEMBE SEKONDARI
S. L. P. 114
NJOMBE

ONE STEP DOES NOT MAKE A PATH